



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA



Tarehe 25/05/2023

TANGAZO

MWALIKO WA KUMPATA FUNDI MJENZI (local fundi)

KAZI: UJENZI WA JENGO LA UTAWALA (ADMINISTRATION BLOCK)-SINGLE STOREY BUILDING

1. Mwaliko huu wa Kotesheni unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya **[HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA]** kwa Mwaka 2022/2023 wa fedha unaoonekana katika TANePS kwa kazi inayotangazwa kama ifuatavyo:

NA	KAZI	NAMBA YA ZABUNI
1.	UJENZI WA JENGO LA UTAWALA (ADMINISTRATION BLOCK) - SINGLE STOREY BUILDING	LGA/109/2022/2023/W/FA/01

2. *Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imepokea/ fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala (Administration block (HQ) - Single Storey Building), na inakusudia kutumia sehemu ya fedha hizi kulipia malipo halali chini ya Mkataba ambao Mwaliko wa Kotesheni hii umetolewa. Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji anaalika mafundi wote kutoka Taasisi za Serikali , watu binafsi ,Vikundi na Mashirika ya umma waombe zabuni kwa wenye sifa zifuatazo:*

- i. Awe anajua kusoma na kuandika
- ii. Awe na vyeti vya fani ya uhandisi Ujenzi kwa ngazi ya daraja la I na kuendelea na amesajiliwa na bodi ya wahandisi (ERB).
- iii. Awe na akili timamu na umri wa Zaidi ya miaka 18
- iv. Asiwe amewahi kushitakiwa na kuhukumiwa kwa kosa lolote la jinai au kuthibitika kushindwa kutekeleza kazi zinazofanana na hii/hizi mahali popote.
- v. Awe na uwezo wa kusoma na kutafasiri Michoro/Ramani/BOQ kwa usahihi
- vi. Awe na uzoefu wa kazi za ujenzi wa majengo makubwa (N: B Mwenye uzoefu wa kujenga majengo yaliyotajwa hapo juu atapewa kipaumbele). Atoe uthibitisho wa kimaandishi kutoka kwa waajiri wasiopungua wawili aliowahi kufanya kazi nao ndani ya miaka 2 (2020-2022)
- vii. Awe na uwezo wa kuajiri mafundi wasaidizi/vibarua na kuwalipa kwa wakati
- viii. Awe na uwezo wa kumiliki au kukodi vitendea kazi muhimu katika ujenzi wa majengo kama Compactor, Dump levels/Levelling Machines, nk).
- ix. Awe na wafanyakazi wenye ujuzi wa maeneo yote yaliyoainishwa kwenye mchoro (Civil Technicians, Architects) vyeti vyao viambatanishwe.
- x. Fundi awe na namba ya Usajili ya mlipa kodi (TIN)
- xi. Awe tayari kulipa tozo za Serikali kama:
 - a) Kodi ya Zui (withholding Tax 5%).
 - b) Ushuru wa Huduma (service levy 0.3%)

Mafundi ujenzi watakaopenda kuomba kazi hii wanatakiwa kuchukua nyaraka za zabuni hii katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kuanzia tarehe 25/05/2023 ya tangazo hili, siku za kazi kuanzia **saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri**

Mafundi ujenzi watakaochukua nyaraka za zabuni, wanatakiwa kusoma nyaraka hizo na kuzielewa, kuzijaza vizuri kwa kufuata maelekezo yaliyomo kwenye nyaraka hizo,

3. Unakaribishwa kuwasilisha Kotesheni (Bei) Kwa ajili ya utoaji huduma Kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika **Sehemu ya Pili**.
4. Kotesheni zote zijazwe kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Kotesheni

[LGA/109/2022/23/W/FA/01 -UJENZI WA JENGO LA UTAWALA na kuwasilishwa kwa KATIBU WA BODI YA ZABUNI – HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA, S.L.P 170, MASWA – SIMIYU.

5. Maombi ya zabuni yatalipiwa kiasi cha Tshs. 100,000.00 (Mia Moja Elfu tu) **Fedha hizi hazitarudishwa**. Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Malipo yatafanyika kwa njia ya kielektroniki kwa kupewa Control Namba katika ofisi ya Mapato .Maombi yote yaambatanishwe na risiti ya kununulia zabuni
6. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni **01/06/2023** kabla ya **SAA 4.30 ASUBUHI** na Kotesheni zitafunguliwa mara tuu baada ya muda wa mwisho wa kupokea katika ukumbi mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.
7. Kotesheni ambazo hazijawasilishwa katika box la kupokelea zabuni au zitakazowasilishwa katika muundo usiokubalika hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yale.

